Ulega atembelea shamba la mifugo hekta 5,633.7

Na SOPHIA NYALUSI, *NANYUMBU*

NAIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, ametembelea shamba la uzalishaji mifugo Nangaramo ambalo lina hekta 5,633.7 lenye mifugo 382 na linaweza kutimiza dhumuni lake la kusambaza mitamba yenye tija kwa wananchi.

Akizungumza jana na wananchi wa Nangaramo, Ulega alisema serikali ina mashamba ya mifugo zaidi ya matano katika mikoa mitano na yote mifugo ipo na inaendelea kujizalisha kwa kasi ili kuongeza mifugo.

Ulega alisema Serikali ya Awamu ya Sita, chini ya Rais Samia Suluhu Hassan, imeandaa bajeti ya matengezo ya Shamba la Nangaramo, litafanyiwa marekebisho ili kuhakikisha uzalishaji unakua kwa kasi.

"Serikali kwa mwaka wa fedha 2021/2022, itanunua mitamba 100 kwa ajili ya kundi la ng'ombe wazazi ili liendelee kujizalisha na kuongeza ng'ombe wengi katika eneo la Nangaramo," alisema Ulega .

Hata hivyo, alimuagiza meneja wa shamba, kuandaa bucha kwa ajili ya uchinjaji ili wananchi wapate kununua kitoweo na kuongeza mapato ya uzalishaji katika shamba la Nangaramo.

"Naomba ujiongeze meneja wa shamba katika kuhakikisha mnatengeza mradi wa kubuni, uzalishaji na kuhakikisha unaandaa bucha kwa ajili ya uzalishaji mkubwa wa Wilaya ya Nanyumbu na Mkoa wa Mtwara," alisema Ulega.

Aliwaomba wananchi wa Nangaramo kuacha kuchoma moto eneo la shamba, waendelee kulilinda kwa kuwa serikali imetenga fedha nyingi kwa ajili ya ukarabati mkubwa.

"Naomba Mkuu wa Wilaya ya Nanyumbu, muende mkakague vizuri eneo hilo la shamba ambalo wananchi wanataka kulima mpunga ili waendelee kulima mashamba na kuongeza pato na chakula katika maeneoyao,"alisema.

Naye Mbunge wa Jimbo la Nanyumbu, Yahaya Mhata, alimpongeza Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi kwa kutatua kero za wananchi wa Nangaramo ambao walikuwa wanaomba ardhi kwa ajili ya kulima mpunga wa chakula.

"Namshukuru Ulega kwa kupokea ujumbe wa kuomba mkopo wa wanawake ambao wanahitaji kujifunza kufuga ng'ombe ili kuendelea kujiongezea kipato katika eneo la Nangaramo na kukuza uzalishaji," alisema Mhata .



SHAMBANI

NAIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, akichunga ng'ombe katika Shamba la Uzalishaji wa Mifugo Nangaramo, Wilaya ya Nanyumbu, mkoani Mtwara, jana. (Picha na Sophia Nyalusi).

Scanned with CamScanner

Wilaya ya Kilindi, akiwa katika ziara mkoani Tanga, juzi. Kushoto ni Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Tanga, Hendry Shekifu . (Picha na Jamal Zuberi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa).

* Mgogoro ardhi Ranchi yaTaifa, wafugaji waisha *

Na FADHILI ABDALLAH, *Kigoma*

RAIS Samia Suluhu Hassan, amemaliza mgogoro wa muda mrefu baina ya wafugaji kutoka mikoa ya kanda ya ziwa na Ranchi ya Taifa ya Malai baada ya kukubali kumega eneo lenye ukubwa wa hekta 6,000 na kuwakabidhi wafugaji hao waweze kulitumia eneo hilo.

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, amelikabidhi eneo hilo kwa halmashauri ya wilaya ya Uvinza kwa niaba ya Rais Samia Suluhu Hassan.

Alisema halmashauri ya Uvinza kwa kushirikiana na kampuni ya Ranchi za Taifa, wanapaswa kuligawa eneo hilo kwa mfugaji mmoja mmoja kwa ajili ya matumizi yao.

Hatua hiyo inafuatia kuwepo mgogoro kati ya wafugaji, Halmashauri ya Wilaya ya Uvinza na Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO).

Zaidi ya wananchi 5,900, walidaiwa kuvamia eneo la ranchi kuanzia mwaka 2018, kisha kuendelea na shughuli za ufugaji na kilimo.

Kufuatia hatua hiyo ya serikali, Waziri Ndaki, alisema Rais Samia, alishauriwa kutoa hekta 4,000, lakini baada ya kufanywa kwa sensa ya watu na mifugo, aliamua kutoa hekta 6,000 ziweze kutumiwa na wananchi.

Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya Ranchi za Taifa, Profesa Peter Msoffe, alisema mchakato umefanyika kwa kuwa na vikao zaidi ya vitano ambavyo vilihusisha wawakilishi wa wizara ya mifugo na uvuvi, viongozi wa halmashauri ya wilaya Uvinza na Kasulu, viongozi wa serikali za vijiji na viongozi wa wananchi hao waliovamiana, changamoto mbalimbali zilijitokeza.

Msofe alieleaza licha ya mapendekezo na ushauri uliotolewa na wataalamu, wananchi hao walikuwa na mapendekezo, ushauri na maamuzi ambayo wakati mwingine yaliegemea katika baadhi ya makundi kuona yananufaika zaidi.

"Kwa sasa, kumekuwa na idadi kubwa ya watu na mifugo, hiyo inatokana na ongezeko la wavamizi hao, baada ya kusikia umeanza mchakato wa sensa na upimaji, baadhi ya watu waliongezeka ambao awali hawakuwepo katika eneo hilo," alisema Mkurugenzi huyo wa NARCO.

Alisema eneo hilo la hekta 6,000 limegawanywa kwa hekta 2,500 kutoka kitongoji cha Kazaroho katika kijiji cha Mpeta na hekta 3,500, kitongoji cha Mwanduhu Bantu kijiji cha Mpeta, wilaya ya Uvinza.

Mkurugenzi huyo wa NARCO, alisema eneo lote la Ranchi hiyo lina ukubwa wa hekta 500, vipo vitalu 56 ambavyo vinakodishwa kwa wananchi wafugaji kwa ajili ya kufuga na kuchunga mifugo kibiashara kwa wananchi kulipa sh. 3,500 kwa hekta moja.

MGOGORO

RANCHI

Alisema halmashauri ya Uvinza kwa kushirikiana na kampuni ya Ranchi za Taifa, wanapaswa kuligawa eneo hilo...

Scanned with CamScanner

Wananchi wakabidhiwa eneo walilopewa na Rais Samia

Na Fadhili Abdallah, Kigoma

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, amekabidhi kwa Halmashauri ya Wilaya ya Uvinza eneo lenye ukubwa wa hekta 6,000 lililotolewa na Rais Samia Suluhu Hassan kwa wananchi wa kijiji cha Mpeta na Chakuru.

Eneo hilo lililo ndani ya Hifadhi ya Ranchi ya Taifa ya Malai, limekabidhiwa kwa halmashauri ili ligawiwe kwa wananchi hao, wafanye shughuli za ufugaji baada ya mgogoro wa muda mrefu kati yao na serikali.

Rais Samia aliamua eneo hilo kumegwa kutoka hifadhi hiyo baada ya kusikiliza kilio cha wafugaji hao kutoka mikoa ya Kanda ya Ziwa walioeleza kutokuwa na maeneo kwa ajili ya mifugo yao.

Kabla ya kukabidhi eneo hilo, serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi, watendaji wa halmashauri za wilaya Uvinza na Kasulu kutoka idara za ardhi, kilimo na mifugo, walifanya sensa kujua idadi ya waliovamia.

Ndaki alisema kuwa awali Rais Samia alishauriwa kutoa hekta 4,000 lakini baada ya sensa hiyo ya watu na mifugo, aliamua kutoa hekta 6,000 zitumiwe na wananchi hao.

"Baada ya Rais Samia Suluhu Hassan kutoa eneo hili naomba kutangaza kuwa serikali haitaongeza eneo lingine na mgawanyo utafanywa kwa watu zaidi ya 5,900 waliokuwa wakihusika na mgogoro na kwamba watakaovamia eneo la ranchi ambalo si eneo lililomegwa na kugawiwa, sheria itachukua mkondo wake," alisema.

Akitoa taarifa kwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya Ranchi za Taifa (Narco), Profesa Peter Msoffe, alisema kuwa mchakato umefanyika kwa kuwa na vikao zaidi ya vitano.

Vilihusisha wawakilishi wa wizara, viongozi wa halmashauri ya wilaya Uvinza na Kasulu, viongozi wa serikali za vijiji na viongozi wa wananchi hao waliovamia.

Msofe alisema kuwa eneo hilo la hekta 6,000 limegawanywa kwa hekta 2,500 kutoka Kitongoji cha Kazaroho katika Kijiji cha Mpeta na hekta 3,500 Kitongoji cha Mwanduhu Bantu Kijiji cha Mpeta Wilaya ya Uvinza.

Mkurugenzi huyo wa Narco, alisema kuwa eneo lote la ranchi hiyo lina ukubwa wa hekta 500 na kuna vitalu 56 ambavyo vinakodishwa kwa wananchi wafugaji kwa ajili ya ufugaji na uchungaji wa mifugo kibiashara. Wanalipa Sh 3,500 kwa hekta moja ambayo atakodi kwa mwaka.

Akizungumza katika mkutano huo, Mkuu wa Wilaya ya Uvinza, Anafi Msabaha, alisema kuwa mgogoro huo umefikia mwisho kwa uamuzi wa rais kutoa eneo ambalo litatumiwa na wananchi waliokuwa kwenye mgogoro.

Alisema wilaya itasimamia kuona taratibu za ugawaji zinafanyika kwa uwazi na wananchi wafugaji waliohusika wanapatiwa maeneo kulingana na mgawanyo utakaofanyika.

Mmoja wa wananchi, Masele Mayenga, alisema kuwa eneo lililotolewa linaweza kutumika kupatia ufumbuzi wa mgogoro uliokuwepo.

Kwa mujibu wa wananchi, wafugaji walikuwa wakisumbuliwa na kuondolewa eneo la ranchi kwa kuvamia eneo hilo.

Scanned with CamScanner